**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI J.M. KIKWETE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu**

**MkuuwaShule: 0766 205 346.**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0675 393 259.**
**Matron:0759 522 632.**
**ShuleyaSekondari J.M.KIKWETE,**

**S.L.P 190,**


**Tarehe…………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………..**

**S.L.P……………………………………..**

**…………………………………………….**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO C H A TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI J.M. KIWETE HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA MKOA WA SONGWE MWAKA ……………...**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya HKL/HGL

Shule ya Sekondari J.M.KIKWETE ipo pembezoni wa barabara iendayo kata ya Mpande, umbali wa kilometa 1 kutoka stand ya Sogea, umbali wa kilometa 5 kutoka Standi kuu ya mabasi ya Mpemba. Ukifika stendi kuu ya mabasi **Mpemba**, unapanda bajaji kwa gharama ya Tsh 1,500/= au Tsh. 700/= kwa daladala mpaka stendi ya Sogea, utapanda bajaji Tsh. 500/= au boda boda kwa Tsh. 1,000/= toka Stendi ya sogea mpaka shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe…………………hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………………..Mwisho wa kuripoti ni tarehe…………………………….

**2.** **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**A. Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni sketi ya rangi ya **Peacock Blue** (moja) na **Army Green** (moja). Sketi inatakiwa iwe na rinda box mbele na nyuma, marinda matatu ya kawaida kushoto na kulia. Urefu wa sketi ufike kwenye kifundo cha mguu.



ARMY GREEN
( SKIRT)



PEACOCK BLUE
( SKIRT)

ii. Mashati mawili ya mikono mirefu rangi nyeupe
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni **NYEUPE** na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (kwa waislamu)
iv. Sare ya Michezo ni jezi full yenye rangi ya nyekundu (moja) na Truck suit rangi ya **DARK BLUE** yenye mistari mweupe pembeni isiyobana (moja). Pamoja na raba nyeupe jozi moja;
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi ndefu jozi mbili nyeupe za shule;
vii. Sweta ni rangi ya **DARK BLUE** (mawili);
viii. Tai mbili, pundamilia rangi ya peacock blue (moja) na pundamilia rangi ya army g reen (moja) (ndefu);
ix. Tisheti (T-shirt) ni rangi ya kijivu (Gray) yenye kola na mfuko upande wa kushoto– (Zinaweza kupatikana shuleni) kwa Tsh. 15000/- tu

**B. Nguo za kazi (Shamba dress)**

Rangi ya draft ndogo rangi nyeusi na damu ya mzee mshono wa solo (magauni mawili yawe marefu mpaka chini) (angalia rangi imeambatanishwa hapa chini)



DRAFT NDOGO NYEUSI NA DAMU YA MZEE

( SHAMBA DRESS)

**3. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja Nayo shuleni:-**

i. Madaftari tisa 3Q na 4Q
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo vya tahasusi husika. **(rejea orodha ya vitabu iliyoambatanishwa mwishoni mwa fomu hii)**
iv. Scientific Calculator; (kwa wanaosoma Geography)
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe ni futi $2\frac{1}{2}$ x 6

vi. Mashuka Jozi 2 ya rangi blue bahari na Pinki, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 nyeupe.
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli,kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 zenye mifuniko; (Lita 20 mojana Lita 10 moja)
x. Kwanja 1 (HKL), jembe 1 (HKL, HGK), reki 1(HGK), mifagio 3 ya ndani (soft bloom (HGK), hard bloom (HKL) na brush za chooni (HKL)) pamoja na Mopa moja (HGK).

**NB. Kama unatokea mbali vifaa kama magodoro, vifaa vya usafi na stationaries vinapatikana shuleni.**

## 4. Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB.Michango yote ilipwe kupitia akaunti ya shule ya NMB 61201100062 JINA LA AKAUNTI – J.M. KIKWETE SECONDARY SCHOOL RECURRENT ACCOUNT**

- **Mwanafunziaje na Bank payslip.**
- **Mwanafunzi aje na BIMA ya afya au TSHS. 50,400/=**

## 5. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## A. Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wa kati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- **Mzaziharuhusiwikumtembeleamtotoisipokuwakwa sababu maalum tu.**

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

(i) Wizi;
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
(vi) Kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
(viii) Uvutaji wa sigara;
(ix) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuolewa;
(x) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xii) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yashule;
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa;
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
(xvi) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 6. Viambatanisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi pamoja na Namba zao za Simu.

**7.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule: HAMZA ATHUMAN MAHAMUDU**

**Muhuri wa Mkuu wa Shule** 


**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0766 205 346**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0675 393 259**
- **Mwandamizi Taaluma: 0753188328**
- **Mwandamizi Malezi: 0759522632**

**UTHIBITISHO WA URAIA WA MTANZANIA**

Nadhibitisha kuwa ........................................................................................ (jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa/kwa kuandikishwa

Baba yake (jina kamili) ……………………………………………………………………………………………………. Amezaliwa katika mkoa wa………………………………..….Wilaya ya ……………………..………………… Tarafa ya ………………………………………………. Kata ya ……………………………………………………

Mama yake (jina kamili) ……………………………………………………………………………… Amezaliwa katika kata ya……………………………………….. Wilaya ya ……………………………

……………………………………………………………

**MKUU WA WILAYA**

**NB**:kila mwanafunzi atalazimika kuishughlikia hati kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni.

**AU LETA NAKALA YA CHETI CHA KUZALIWA BADALA YA FOMU HII**.

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

To…………………………………

**THE MEDICAL OFFICER**

Please examine…………………………………………………………………………………. As to her fitness for pursuing further education at this school.

- Hemoglobin……………………………………………………………………………………………………
- P.V.Blooding…………………………………………………………………………………………………
- (A)Blooding…………………………………………………………………………………………………

  (B)Hearing ……………………………………………………………………………………………………
- Blood Pressure………………………………………………………………………………………………
- Urine for Sugar and Pregnancy tests…………………………………………………………………………
- Stool for urine examination…………………………………………………………………………………
- Asthma…………………………………………………………………………………………………………
- Skin diseases

  ……………………………………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………………………………
- Leprosy…………………………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………………………………
- Pulmonary tuberculosis ……………………………………………………………………………………
- Employs ………………………………………………………………………………………………………
- Deformity……………………………………………………………………………………………………
- Mental problem

  ……………………………………………………………………………………………………………
- Comments……………………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………………………………

  ……………………………………………………………………………………………………………………

  DESIGNATION

  ...................................................... Stamp .........................................

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**SHULE YA SEKONDARI J.M. KIKWETE**

FOMU YA KUKUBALI NA FASI

**a. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwafunzi mwenyewe)** Jina kamili (kama alivyosajili wa darasala saba)………………….……………………………… Tarehe ya kuzaliwa……………..…Kabila…………………dini na dhehebu…………………… shulenitokayo……………….…………Mahali niishipo…………….…………..

Mkoa……………………..…Anuani…………………….…………………

Jina la baba/mlezi…………………………………….kazi yake………………………….. Jina la mama/mlezi……………………………………...kazi yake…………………………… Wazazi/walezi wanaishi (wapi)…………………………pamoja/au wametengana…………… Anuani ya mzazi/mlezi……………………………..simu…………………………………… Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje)……………………………wapi……………………… Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi;

Sahihi ya mwanafunzi……………………………….tarehe……………………………… KUKUBALI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi.........................................................................................................................................nimesoma Maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

**b. IJAZWE NAMZAZI AUMLEZI**

Mimi……………………………………………………………. ambaye ni …………………….wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika fomu ya kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, naahidi kumpa mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika.

Anuaniyanguyakudumu……………………………..simu……………………………… Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Nathibitisha Taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli

Sahihi ya mzazi /mlezi……………...

**SHULE YA SEKONDARI J. M. KIKWETE MAHITAJI YA VITABU VYA KIDATO CHA V-…………………..**

Tunashauri baadhi ya vitabu vifuatavyo vinunuliwe kulingana na masomo atakayosoma mwanafunzi na vitabu hivi ni mali ya mwanafunzi.

## 1. HISTORY

i. Adu Boherin, (ed) General History of Africa VII Africa under colonial domination 1880-1953
ii. David Wrouh: Modern world History
iii. Carton J.H Hayes contemporary Europe since 1870-1958
iv. Denis Richard: An Illustrated history of modern Europe 1789-1984 7th edition (1985)
v. Walter Dodney: How Europe under developed Africa
vi. L.E Snell grove: Africans: The history of continental low price edition (1999)
vii. Michael Tiddy: General history of Africa
viii. Kelvin shillington: History ofAfrica

## 2. ENGLISH LANGUAGE II

- **NOVELS & SHORT STORIES**

i. THE BEAUTIFUL ONES ARE NOT YET BORN – AYIKWE IARMAH
ii. A MAN OF THE PEOPLE – CHINUA ACHEBE
iii. HIS EXCELLENCY THE HEAD OF STATE – DANNYSAFO
iv. A SEASON OF WAITING – DAVID OMOWALE
v. ENCOUNTER FROM AFRICA – MACMILIAN EDUCATION
vi. BLACKMAMBA– JOHN

- **POEMS**

i. A WOUNDERFUL SURGEON AND THE POEMS– CHARLES MLOKA
ii. SELECTED POEMS –INSTITTUTE OF EDUCATION

- **PLAYS**

i. BETRAYAL IN THE CITY– FRANSIC IMBUGA
ii. I WILL MARRY WHEN I WANT –NGUGI WA THIONG'O & NGUGI WA MIRII
iii. AN ENEMY OF THE PEOPLE – HENRICK IBSEN
iv. DIVINE PROVINCE–SEVERIN NDUNGURU
v. THE BRIDE– OSTINU KENYA
vi. LWANDA MAGERE –OKOITI OMTATAH

## 3. ENGLISH STRUCTURE (ENGLISH LANGUAGE)

i. An introduction to language –Masija S.J
ii. Advanced level English, Practice Approach New Syllabus Nicodemus Asheli
iii. Grammar and composition Handbook Gleoncoe McGrowthl

iv. Speech communication Yu edition WilliamB rooks/Robert W.Leath
v. Communication skills theory and practice (Michael Kadeghe)

## 4. GEOGRAPHY

i. General Geography by R.BBunnet
ii. Practice Geography for Africa by Pritchard John M.
iii. Regional focal studies for Advance by Msabila D.T
iv. Map reading by McMaster
v. Physical Geography by Msabila D.T
vi. Geography an integrated approach by David Waugh

## 5. KISWAHILI

i. Jitayarishe kwa fasihi ya Kiswahili, kidato cha V na VI
ii. Mwongozo wa kujibu maswali vitabu teule V & VI
iii. Kamusiya Kiswahili sanifu

- **MASHAIRI**

i. KIMBUNGA– HAJIGORA
ii. MAPENZI BORA–SHAABAN ROBERT
iii. CHUNGU TAMU–THEOBALD MVUNGI
iv. FUNGATE YA UHURU–MOHAMED KHATIB

- **RIWAYA**

i. USIKU UTAKAPOKWISHA – MBUNDA MSOKILE
ii. KUFIKIRIKA–SHABAAN ROBERT
iii. MFADHILI – HUSSEIN TUWA
iv. VUTAN; KUVUTE–SHAFII ADAM SHAFII

- **TAMTHILIYA**

i. KWENYE UKINGO WATHIM – EBRAHIM HUSSEIN
ii. MORANI – EMMANUEL MBOGO
iii. KIVULI KINAISHI – SAID MOHAMED
iv. NGUZO MAMA – PENINA MHANDO